KARATASI YA TAARIFA

nystateofhealth
The Official Health Plan Marketplace



TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

# Mabadiliko ya Bima ya NY State of Health Wakati wa Dharura ya Virusi vya Korona

**Usiondoke bila bima.**

**NY State of Health ni bima rasmi ya afya ya New York Marketplace.**

**Tupo hapa kusaidia.**

**Tuma Ombi Sasa.**

Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov

Kwa simu kupitia 1-855-355-5777
TTY: 1-800-662-1220

Ungana na Msaidizi wa Usajili kwenye info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho na jimbo zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsia, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

## Kuwa na bima ya afya ni muhimu. Wakati huu kuliko wakati mwingine.

**NY State of Health imechukua hatua nyingi ili kusaidia wakazi wa New York ambao hawana bima au wanaopoteza bima ya mwajiri.**

### Maswali Yanayoulizwa Sana:

### Mabadiliko ya Mapato na Upotezaji wa Bima ya Mwajiri :

**Je, ninapaswa kufanya nini nikipoteza bima ya afya ya mwajiri wangu au ikiwa siwezi kumudu COBRA inayotolewa na mwajiri wangu?**

- Huenda ukastahiki usaidizi wa kulipia bima ya afya kupitia NY State of Health, au kwa bima ya bila malipo.
- Usisubiri kutuma ombi. Unapaswa kutuma ombi ndani ya siku 60 baada ya kupoteza bima yako ili kuhakikisha kuwa unaweza kujisajili katika bima mwaka huu.

**Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa mapato yangu yamebadilika na tayari nimejisajili kwenye bima kupitia NY State of Health? Je, ninaweza kupata usaidizi zaidi wa kulipia bima yangu?**

- Unaweza kustahiki usaidizi wa kulipia bima yako. Sasisha akaunti yako kwa mapato yako mapya ndani ya siku 60 baada ya mabadiliko.  Huenda ukastahiki kwa usaidizi zaidi wa fedha unaoweza kupunguza gharama ya bima yako.

TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

# Mabadiliko ya Bima ya NY State of Health Wakati wa Dharura ya Virusi vya Korona

## Je, Sheria ya Coronavirus Aid, Relief and Economic Security (CARES) Act?

Coronavirus Aid, Relief and Economic Security (CARES) Act ilipitishwa na Bunge na kutiwa sahihi kuwa sheria na Rais Trump tarehe 27 Machi, 2020. Mpango huu wa msaada wa uchumi wa trilioni $2.2 ulipitishwa ili kulinda wamarekani kutokana na athari za afya ya umma na uchumi zinazosababishwa na COVID-19. Sheria ya CARES inatoa usaidizi wa uchumi kwa wafanyakazi, familia, na wafanyabiashara wadogowadogo wa Marekani na inalenga kuhifadhi kazi kwa tasnia za Marekani.

## Malipo MAPYA ya Mapato ya Serikali Kuu/Fidia ya Kukosa Ajira Kutokana na COVID:

**Nilipokea malipo kutoka kwenye Sheria ya serikali kuu ya CARES (maarufu kama malipo ya kichangamsho). Je, kiasi hiki cha pesa kinachukuliwa kama mapato katika ombi langu la NY State of Health?**

- Hapana. Malipo ya kichangamsho hayachukuliwi kama mapato ya mtumiaji yeyote wa NY State of Health. Watumiaji wanaostahiki watapokea malipo ya mara moja kutoka U.S. Department of the Treasury. Malipo haya yanasambazwa chini ya sheria ya serikali kuu, inayojulikana kama Sheria ya CARES, iliyoidhinishwa ili kukabiliana na janga la COVID-19. Watumiaji wanaostahiki watapokea malipo ya mara moja ya $1,200 kwa kila mtu mzima na $500 kwa mtoto.

**Ninapokea Pandemic Unemployment Compensation kutoka kwenye jimbo mbali na manufaa yangu ya kawaida ya kukosa ajira. Je, ninapaswa kuyaripoti kama mapato ninapotuma ombi la bima ya afya kupitia NY State of Health?**

- Inategemea na wewe. Malipo ya mpango wa Pandemic Unemployment Compensation ($600 kwa wiki) yanachukuliwa kama mapato kwa baadhi ya wasajiliwa wa NY State of Health, lakini si kwa wengine.
- Ripoti Malipo ya mpango wa Fidia ya Kukosa Ajira kutokana na Janga (Pandemic Unemployment Compensation) yako ikiwa:
    - Huna watoto* kwenye kaya yako, NA
    - Mapato yako ya kila mwaka ni zaidi ya $25,520 kwa mtu mmoja au $34,480 kwa wanandoa.
- USIRIPOTI Malipo ya mpango wa Fidia ya Kukosa Ajira kutokana na Janga (Pandemic Unemployment Compensation) yako Ikiwa:
    - Una watoto.*
    - Mapato yako ya kila mwaka ni chini ya $25,520 kwa mtu mmoja au $34,480 kwa wanandoa.
- Ikiwa unahitaji kusasisha ombi lako ili uongeze Pandemic Unemployment Compensation as income, NY State of Health Assistors and Customer Service zinapatikana ili kukusaidia kukamilisha ombi.

**Neno "watoto " linamaanisha mtoto chini ya miaka 19, au 19 na 20 ikiwa ni mwanafunzi wa kutwa.*

TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

# Mabadiliko ya Bima ya NY State of Health Wakati wa Dharura ya Virusi vya Korona

## Vipindi vya Nyongeza ya Kulipa na Kulipia Bima:

**Ninajisajili katika Essential Plan (EP) na nina $20 ada ya bima kila mwezi.  Je, ninahitaji kutoa ada yangu ya kwanza ya bima ndani ya siku 10 ili bima yangu kuanza?**

- Wakati wa kipindi cha dharura cha Virusi vya Korona, mipango ya afya itakupa kipindi kirefu cha kutoa malipo yako ya kwanza ya $20.  Unapaswa kuzungumza na mpango wa afya uliojisajili kwao.

**Ninasjisajili katika Qualified Health Plan (QHP).  Je, ninahitaji kutoa ada yangu ya kwanza ya bima ndani ya siku kumi za tarehe ya kuanza ya bima yangu?**

- Ndiyo.  Wasajiliwa wote wa QHP, wakiwemo wale wanaolipa ada ya yote ya bima ambao wanapokea APTC, wanahitajika kulipa malipo ya kwanza ya ada ya bima yao ili bima yao ianze. Mipango mingine inaweza kuongeza kipindi cha siku 10.  Unapaswa kuzungumza na mpango wa afya unaojisajili kwao.

**Tayari nimejisajili kwenye Qualified Health Plan na kupata usaidizi wa kulipia bima na APTC.
Je, ninapaswa kulipa ada ya bima yangu ya kila mwezi kwa muda gani?**

- Wakati wa dharura ya Virusi vya Korona, kipindi cha muda ambacho unapaswa kulipia bima yako ya kila mwezi, kinachoitwa "kipindi cha nyongeza ya kulipa", kimeongezwa kutoka siku 90 hadi 120.  Huhitaji kuonyesha kuwa una changamoto ya fedha ili ustahiki kuongezwa kipindi cha nyongeza ya kulipa. Ankara unayopokea kutoka kwenye mpango wako wa afya itaonyesha tarehe za malipo yako.
- Usipolipa ada yako ya bima kipindi hiki cha nyongeza ya siku 120, mpango wako wa afya unaweza kuhitimisha bima yako siku ya 60 ya kipindi cha nyongeza ya kulipa na hutakuwa na bima kwa huduma yoyote uliyotumia baada ya tarehe hiyo na huenda usiweze kupata bima kwa mwaka uliosalia, isipokuwa uwe na tukio la maisha linalostahiki linalochochea SEP.
- Ikiwa unatatizika kulipia bima yako, wasiliana na NY State of Health, au zungumza na mpango wako wa afya.  Huenda kukawa na chaguo nafuu zaidi kwako.
- ***Dokezo:*** NYS Department of Financial Services imetoa mwongozo kwa watu binafsi wanaolipa ada yote ya bima.  Uthibitisho wa changamoto ya COVID-19 unahitajika kwa idadi hii ya watu.